# Ujumbe Muhimu/Kitaalam: Ulinzi wa Watoto Katika Kipindi cha Ugonjwa wa Corona. (Chapisho.1)[1]



*Picha na: UNICEF/Leonardo Fernandez/India 2019*

## Utangulizi

Magonjwa ambukizi kama COVID-19 yanaweza kuvuruga mazingira ambamo ukuaji na maendeleo ya mtoto hutokea. Kuvurugika kwa familia, urafiki, utaratibu wa kila siku, na jamii kwa ujumla kunaweza kuwa na athari mbaya kwa ustawi wa watoto, ukuaji, na uangalizi. Kwa kuongezea, hatua zinazotumiwa kuzuia na kudhibiti kuenea kwa COVID-19 zinaweza kuweka watoto katika hatari za uangalizi. Hatua za majumbani, hatua za utumiaji vifaa maalumu, kuanzisha karantini kwa kanda mbalimbali na hatua za kujitenga zinaweza kuathiri vibaya watoto na familia zao.[2]

[1] Rejea pendekezwa: The Alliance for Child Protection in Humanitarian Action, Technical Note: Protection of Children during the Coronavirus Pandemic, Version 1, March 2019

[2] Kwa taarifa Zaidi juu ya karantini tembelea kurasa 14–15 za Mwongozo: Ulinzi wa Mtoto katika kipindi cha mlipuko wa magonjwa ambukizi

Madhumuni ya muhtasari huu ni kusaidia watendaji wanaojihusisha na ulinzi wa watoto kukabiliana vyema na hatari za kulinda watoto wakati wa janga la COVID-19. Sehemu ya 1 inawasilisha hatari kuu za ulinzi wa watoto ambazo watoto wanaweza kuzipata kutokana na COVID-19. Sehemu ya 2 inawasilisha chaguzi za kimfumo zinazoambatana na Viwango vya chini vya Ulinzi wa watoto katika hatua ya Haki za Binadamu *(CPMS)-2019 (2019 Minimum Standards for Child Protection in Humanitarian Action (CPMS))* na Ujumbe Elekezi: Ulinzi wa Watoto Wakati wa Mlipuko wa Magonjwa Ambukizi *(Guidance Note: Protection of Children During Infectious Disease Outbreaks).*

# 1. Ulinzi wa watoto katika muktadha wa virusi vya corona


COVID-19 inaweza kubadilisha kwa haraka sana muktadha ambao watoto wanaishi. Njia za kuwaweka watu katika karantini pamoja na kufunga mashule na kuzuia mizunguko ya watu huvuruga utaratibu wa kila siku wa watoto na msaada wa kijamii, wakati pia huleta mafadhaiko mapya kwa wazazi na walezi ambao watalazimika kufuata njia mpya za utunzaji wa watoto au kuacha kazi. Unyanyapaaji na ubaguzi unaohusiana na COVID-19 unaweza kuwafanya watoto kuwa katika hatari ya vurugu na dhiki ya kisaikolojia. Hatua za kudhibiti magonjwa ambazo hazizingatii mahitaji maalum ya kijinsia na udhaifu wa wanawake na wasichana zinaweza pia kuongeza hatari zao za ulinzi na kusababisha njia mbaya za kukabiliana. Watoto na familia ambazo tayari ziko katika mazingira magumu kwa sababu ya hali duni ya kiuchumi na kijamii au kwa wale ambao wanaishi katika mazingira yaliyojaa watu wengi wako katika hatari kubwa.

## 1.1. Athari ya Kijamii na Kiikolojia ya COVID-19

Kuyumba kwa jamii; kuvurugika au upatikanaji mdogo wa huduma muhimu za kijamii.

Kuvunjika kwa imani; kugombania rasilimali chache; upatikanaji duni wa huduma za msaada, elimu na nafasi za kucheza.

Kutengana kwa wanafamilia, upatikanaji duni wa huduma za msaada wa kijamii, kuongezeka kwa ukatili/unyanyasaji wa watoto nyumbani.




Hatari kwa mtoto anaeonewa, alietelekezwa, aliefanyiwa ukatili na unyonyaji, mwenye matatizo ya kisaikolojia na kuleta athari mbaya katika maendeleo.

Unyanyapaaji wa makabila fulani.

Kuvuruga maisha; kuvuruga uhusiano na msaada wa kifamilia; hofu ya ugonjwa.

## 1.2. Hatari za Ulinzi wa Mtoto

Baadhi ya hatari za kulinda watoto zifuatazo hapa chini zinaonekana katika janga la sasa la COVID-19 na zingine ni hatari zilizoonekana katika milipuko ya magonjwa ya kuambukiza ya zamani.

| Hatari zilizosababishwa na COVID-19 na njia mahususi za udhibiti | Chanzo cha Hatari |
|---|---|
| **Hatari ya Ulinzi wa Mtoto: Unyanyasaji wa kimwili na kihisia** | |
| • Kupungua kwa usimamizi na kutelekezwa kwa watoto<br>• Kuongezeka kwa unyanyasaji wa watoto na ugomvi ndani ya familia/ kati ya watu<br>• Sumu, hatari nyingine na hatari za majeraha kwa watoto<br>• Shinikizo juu ya au ukosefu wa huduma za ulinzi wa watoto | • Kufungwa kwa vituo vya kulelea watoto/shule, kuendelea kuhitajika kwa majukumu ya walezi wa watoto, magonjwa, kuwekwa karantini / kutengwa kwa walezi wa watoto<br>• Kuongezeka kwa shida ya kisaikolojia kati ya walezi na wanajamii<br>• Upatikanaji na matumizi mabaya ya dawa za kuua viuatilifu na pombe<br>• Kuongezeka kwa vizuizi katika kuripoti matukio |
| **Hatari ya Ulinzi wa Mtoto: Ukatili wa Kijinsia** | |
| • Kuongezeka kwa hatari ya unyonyaji wa ngono kwa watoto, ikiwa ni pamoja na kuomba ngono kwa kigezo cha kumsaidia mtoto, biashara ya ngono na ndoa za utotoni<br>• Shinikizo au ukosefu wa huduma za ulinzi wa watoto / ukatili wa kijinsia | • Kupungua kwa ulinzi wa watoto katika familia<br>• Kupungua kwa mapato ya kaya na / au kutegemea watu wa nje kuleta bidhaa na huduma kwa jamii<br>• Kuongezeka kwa majukumu ya nyumbani wanayopewa wasichana kama vile kutunza familia au kufanya kazi za nyumbani<br>• Jinsia ya watoto wa kike kupewa majukumu ya familia Kama kutunza familia au kufanya kazi za nyumbani.<br>• Kuongezeka kwa vizuizi wakati wa kuripoti matukio na kutafuta matibabu au msaada mwingine |
| **Hatari ya Ulinzi wa Mtoto: Afya ya akili na matatizo ya kisaikolojia** | |
| • Huzuni kwa watoto kwa sababu ya kifo, ugonjwa, au kutengwa kwa mpendwa wao au kuwa na hofu ya magonjwa<br>• Kuzorota kwa hali ya afya ya akili waliyokuwanayo watoto<br>• Shinikizo au ukosefu wa huduma za MHPSS | • Kuongezeka kwa viwango vya msongo kutokana na kutengwa kwenye vyumba vya matibabu au kwenye karantini nyumbani<br>• Watoto na wazazi/ walezi waliokuwa na matatizo ya afya ya akili kabla wanaweza kukosa kupata msaada Kama kawaida au matibabu.<br>• Hatua za kuwaweka karantini zinaweza kuleta woga na hofu katika jamii, hasa kwa watoto, ikiwa hawaelewi kinachotokea |

| Hatari zilizosababishwa na COVID-19 na njia mahususi za udhibiti | Chanzo cha hatari |
|---|---|
| **Hatari ya Kulinda Mtoto: Kazi kwa watoto wadogo** | |
| ● Kuongezeka kwa ushiriki wa watoto katika kazi hatarishi au kujihusisha katika shughuli nyonyaji. | ● Kupotea au kupungua kwa kipato cha kaya<br>● Fursa au matarajio ya kufanya kazi kwa sababu ya kufungwa kwa shule |
| **Hatari ya Ulinzi wa Mtoto: Watoto wasioongozana na walezi/wazazi au waliotengwa** | |
| ● Kusambaratika kwa wanafamilia<br>● Kutokuwa na uangalizi au mtoto kuwa mkuu wa kaya<br>● Kuwekwa na kulelewa katika taasisi | ● Kupoteza kwa wazazi / walezi kwa sababu ya ugonjwa<br>● Kutengwa / walezi kuwekwa karantini mbali na mtoto/watoto<br>● Wazazi kuwapeleka watoto mbali kuishi na familia nyingine katika maeneo ambayo hayajaathiriwa na ugonjwa. |
| **Hatari ya Ulinzi wa Mtoto: Kutengwa na jamii** | |
| ● unyanyapaaji wa kijamii kwa watu walioambukizwa au watu / vikundi vinavyoshukiwa kuambukizwa<br>● Kuongezeka kwa hatari / msaada mdogo kwa watoto wanaoishi / wanaofanya kazi mitaani na watoto wengine ambao tayari wako kwenye hatari<br>● Kuongezeka kwa hatari / msaada mdogo kwa watoto wanaokinzana na sheria, pamoja na wale waliowekwa kizuizini | ● Ubaguzi wa kijamii na ubaguzi wa rangi kwa watu / vikundi vinavyoshukiwa kuambukizwa<br>● Athari kubwa zaidi kwa watu wenye shida zaidi au ulemavu na vikundi vya watu waliotengwa<br>● Kufungwa / kukosa huduma za msingi kwa watoto na / au familia dhaifu<br>● Kuvuruga utaratibu wa kusajili watoto waliozaliwa kutokana na watu kuwekwa karantini |

# 2. Mwitikio wa Ulinzi Kwa Watoto

Kufanya utetezi kwa kushirikiana na serikali, kushirikiana na sekta zingine, na programu maalum za kulinda watoto ni vipaumbele muhimu wakati wa mapambano dhidi ya COVID-19.

## 2.1. Kufanya kazi katika sekta mbalimbali kwa kushirikiana na serikali

Kama ilivyooneshwa katika CPMS, "kuzuia na kukabiliana na milipuko ya magonjwa ya kuambukiza kunahitaji uratibu na ushirikiano kati ya sekta kadhaa." Mwitikio wa sekta nyingi, (a) inahakikisha kuwa mahitaji ya watoto na walezi yanashughulikiwa kwa jumla na (b) husababisha matokeo bora kwa watoto. Washirika wa kazi za Ulinzi wa Watoto pia wanapaswa kuzingatia kushirikiana na viongozi wa dini na viongozi wa jadi. Ujumuishaji wa sekta nyingi unapaswa kuweka kipaumbele:

- Taratibu za kawaida za kuorodhesha na kutoa taarifa juu ya kesi mbalimbali za watoto ambazo zinaweza kuhitaji kufuatiliwa kwa ukaribu;
- Itifaki dhahiri ya kuzuia / kupunguza kutengana kwa familia na aina zingine za hatari za kulinda watoto;
- Kupunguza unyanyapaaji na kutengwa na jamii kutokana na ugonjwa wa COVID-19; na
- Jamii kuratibu na kutoa ujumbe dhahiri na rafiki kwa watoto juu ya hatari za kipekee zinazoweza kuwapata watoto kutokana na mlipuko huu.

Katika kufanya kazi na serikali, washiriki wa Ulinzi wa Mtoto (CP) wanapaswa kutetea kuhakikisha hatua zinazotekelezwa kukabiliana na COVID-19 zinakubaliana na viwango vya kimataifa, zinaendana na ushauri wa WHO, na zinazingatia misingi ya haki za binadamu, hazina ubaguzi badala yake zinazingatia usawa.

Zifuatazo ni hatua zinazopewa kipaumbele katika kufanya kazi na sekta zote pamoja na serikali ili kupata mwitikio mzuri wa shughuli za ulinzi wa watoto.

**AFYA** (Kiwango Na.24 cha CPMS)

- Kutetea watoto walio katika mazingira hatarishi pamoja na familia zao ili wapate huduma za afya pasipo gharama(Ikiwa sera hii si kwa watu wote).
- Kushirikiana kujumuisha matakwa ya Ulinzi wa Mtoto (CP) katika tathmini ya sekta za afya na zana za uchunguzi.
- Kuunda taratibu za kawaida za kuorodhesha na kuripoti kesi za watoto kati ya washiriki wa Ulinzi wa Mtoto na watoa huduma za afya ili kuhakikisha kuwa watoto wanapata huduma salama na inayofaa katika familia zao ikiwa wametengwa.
- Kutetea na kuhamasisha njia thabiti na rafiki kwa watoto za kuwaingiza na taratibu za kuwatoa kwenye karantini ili kuhamasisha umoja katika familia na kupunguza hatari za utengano katika familia.
- Kuwezesha mawasiliano salama na ya kawaida kati ya watoto na wazazi / walezi waliotengwa kwa muda.
- •Kushirikiana kuhakikisha kuna vifaa au huduma za afya ambazo ni rafiki kwa watoto, ikiwa ni pamoja na mwongozo kwa wafanyakazi wa afya juu ya mawasiliano na watoto na hatua maalum za kusaidia ustawi wa kiakili wa watoto wakati wa matibabu na kipindi wakiwa karantini.
- Kusaidia mafunzo ya usalama wa watoto kwa wafanyakazi wa afya (hasa ambapo watoto wametengwa na familia au walezi wao).
- Kuanzisha malalamiko salama, na yenye kupendeza watoto na njia sahihi za utoaji majibu katika vituo vya afya.

- Kuimarisha uwezo juu ya usimamizi wa kitabibu dhidi ya ubakaji na kuhakikisha vifaa vya CMR vinapatikana katika vituo vya afya katika mapambano dhidi ya ukatili wa ngono.
- Kushirikiana juu ya afya ya akili na msaada wa kisaikolojia (MHPSS) na ujumbe kwa watoto na walezi walioathirika na COVID-19.
- Kujumuisha hatua za kulinda watoto wakati wa milipuko ya COVID-19 katika mipango ya dharura.
- Kuhakikisha kuwa taarifa, elimu na vifaa vya mawasiliano (IEC) pamoja na taarifa za huduma zinazopatikana zinazalishwa na kuoneshwa kifupi kwa matoleo rafiki kwa watoto.

**OSHA (WASH)** ( Kiwango Na. 26 cha CPMS)

- Kushirikiana kuhakikisha kuwa vituo vya kunawia mikono vya watoto vinapatikana katika vituo vya afya, shule, vituo mbadala vya kulelea watoto, na maeneo mengine ambayo watoto wanaweza kutembelea.
- Kushirikiana katika shughuli rafiki kwa watoto za kuhamasisha usalama kabla na wakati wa milipuko, ikiwemo uundaji wa mabango na ujumbe wa picha unaowalenga watoto, wazazi / walezi na walimu.
- Kushirikiana juu ya ukaguzi wa usalama ili kutathmini na kushughulikia mahitaji yoyote ya usalama katika vituo vya WASH.

**LISHE (Kiwango Na. 25 cha CPMS)**

- Kuhakikisha watoto na familia zilizowekwa karantini au kujitenga na zile zilizopo katika vituo vya afya wanapata msaada wa kutosha wa lishe.
- Kushirikiana juu ya ukaguzi wa usalama ili kutathmini na kushughulikia mahitaji yoyote ya usalama katika vituo vya lishe.

**ELIMU** (Kiwango Na. 23 cha CPMS; orodha ya rasilimali ya INEE)

- Kupunguza athari za kusimama kwa masomo kwa kutumia njia za mbali za elimu kwa watoto kama vile Runinga, redio au kujifunza mtandaoni.
- Kutetea sambamba na serikali na waajiri binafsi kuwekwa kwa mpangilio rahisi wa kufanya kazi kwa wazazi na walezi ambao wanaweza kuwa wamepoteza huduma ya utunzaji wa watoto ili kuwawezesha kuendelea na utunzaji na elimu ya watoto wao.
- Kufanya kazi na mashule ili kuhakikisha kuwa ujumbe wa ulinzi na usalama unapelekwa kwa wazazi na watoto kwa njia ambayo hupunguza hofu na shida, yenye uhakika na yenye kuhimiza ujumbe wa afya.
- Kuwafundisha waalimu na wafanyakazi wengine wa shule juu ya ishara za dhiki kuwawezesha kutambua na kupeleka watoto ambao wanaweza kuwa na mahitaji maalum ya kinga ya watoto.
- Kuhakikisha kuwa waalimu na wanaojitolea wana maarifa na ujuzi unaofaa kuhusiana na kupunguza hatari ya ukatili wa kijinsia, Uzuiaji wa unyanyasaji wa kijinsia na unyanyasaji (PSEA), usalama wa watoto, njia salama za rufaa
- Kusaidia maendeleo na utoaji wa malalamiko rafiki kwa watoto na njia za mrejesho mashuleni na vifaa vingine vya elimu.
- Kuunda, kusambaza au kuonyesha ujumbe mashuleni kuhusu usalama wa watoto na huduma zinazopatikana ikijumuisha usimamizi wa kesi na utaftaji wa familia na kuziunganisha tena.
- Kufanya kazi na watendaji wa elimu kushughulikia unyanyapaaji na kutengwa kwa watoto mashuleni.

| Matendo ya ulinzi wa mtoto yanayopewa kipaumbele | |
|---|---|
| **Matendo ya Utayarishaji** | **Matendo ya Kukabiliana** |
| ● Washirikishe vijana na watoto, wakiwemo wasichana katika muundo na kuingilia Kati kukabiliana na mlipuko huu. | ● Kufanya uhamasishaji sahihi utakaozingatia tofauti za kijinsia, umbali au umri<br>● Kuboresha njia zilizopo za rufaa |
| **Mkakati wa Ulinzi wa Mtoto: Kuimarisha mazingira ya kifamilia na msaada kwa watoto (Kiwango Na. 16 cha CPMS)** | |
| ● Kufanya kazi na watoto, walezi na wadau wengine kuelewa imani na mazoea ya kitamaduni ambayo yanaweza kulinda au kuhatarisha watoto wakati wa milipuko<br>● Kutambua fursa za kukuza ufahamu ili kuonyesha umuhimu wa uhusiano mzuri baina ya mzazi na mtoto<br>● Kuunda mpango wa mashirika ya pamoja, kwa kushirikiana na mamlaka husika, ili kuimarisha utunzaji wa watoto walio katika mazingira hatarishi. | ● Kutoa msaada katika vituo vya muda vya malezi na familia, pamoja na kaya zinazoongozwa na watoto na kuziwezesha familia kusaidia watoto kukua kihisia na kujihusisha katika njia sahihi za kujitunza<br>● Kutoa msaada wa kifedha na vifaa (pesa au NFI) kwa familia ambazo fursa zao za kujipatia kipato zimeathiriwa<br>● Kuhimiza na kuunda njia salama za kusaidia mawasiliano ya kawaida kati ya watoto na wanafamilia ambao wametengwa<br>● Kufanya kazi na watendaji wengine wa kada, pamoja na serikali, kuweka hatua za kuzuia kuwatenga watoto na familia zao. |
| **Mkakati wa Ulinzi wa Mtoto : Mbinu za Kijamii (Kiwango Na.17 cha CPMS )** | |
| ● Kutambua ni jukumu gani ambalo jamii inaweza kuchukua katika kukuza uelewa na katika kulinda watoto na familia<br>● Kufanya kazi na jamii kutambua mikakati ya kuzuia na kulinda vikundi vilivyo hatarini (mf. wakimbizi, watoto waliopo kwenye malezi mbadala, wale walio katika hatari ya unyanyapaaji na kutengwa na jamii). | ● Kufanya kazi na wanajamii kutengeneza jumbe rafiki kwa watoto juu ya COVID-19, zinazohusiana na hatari na njia za rufaa.<br>● Kutambua mikakati rahisi ya kuwasiliana na jamii kwa mbali<br>● Kwa kushirikiana na jamii, kufanya shughuli za kumaliza unyanyapaaji, kukuza mifumo salama ya kukabiliana, na kusaidia idadi ya watu walioathirika<br>● Kufanya kazi na viongozi wa jadi na kidini kurekebisha mazoea ya kitamaduni, ikiwa ni lazima (i.e. salamu, mazishi na sherehe za kuomboleza, n.k). |

| Mkakati wa Ulinzi wa Mtoto: Utatuzi wa Kesi za COVID-19<br>(Kiwango Na. 18 cha CPMS) | |
|---|---|
| ● Kutoa mafunzo na msaada kwa wahudumu wa kesi na nambari za msaada kwa watoto zilizopo katika kipindi cha COVID-19, zitakazoweza kuwasaidia kupata ukweli na takwimu muhimu, hadithi za uwongo juu ya ugonjwa huu, madhara yake katika Ulinzi wa Mtoto na huduma za msaada | ● Kurekebisha au kuunda upya taratibu za utendaji kwa kushirikiana na sekta ya afya na sekta zingine ili kuhakikisha kuna mbinu salama za utambuzi na utoaji wa rufaa kwa watoto walio katika hatari. |

## 2.2. Programu maalum za Ulinzi wa Mtoto

Je! Ni hatua gani zinazofaa kukamilisha vitendo vilivyopo katika Viwango vya chini vya Ulinzi wa watoto katika hatua ya kibinadamu (Minimum Standards for Child Protection in Humantarian Action) na Kauli ya Mwongozo: Ulinzi wa watoto wakati wa mlipuko wa magonjwa ambukizi (Guidance Note: Protection of Children During Infectious Disease Outbreaks) ili kulinda watoto wakati wa janga la COVID-19? Tofauti na hatari za kukabiliana, lazima tuendeleze juhudi na njia bora za kuishi na jamii, familia, walezi na watoto.

| Matendo ya ulinzi wa mtoto yanayopewa kipaumbele | |
|---|---|
| **Mikakati ya Maandalizi** | **Matendo ya Kukabiliana** |
| **Mkakati wa Ulinzi wa Mtoto (CP):** Kazi za mtu mmojammoja na vikundi kwaajili ya ustawi wa watoto (Viwango vya CPMS 10 & 15). | |
| ● Kwa mashauriano na wengine, tambua njia mbadala za afya ya akili na msaada wa kisaikolojia (psychosocial support) na shughuli za masomo kwa watoto. | ● Toa mafunzo kwa wadau wa afya, elimu, huduma za watoto na MHPSS juu ya hatari zinazohusiana na COVID-19.<br>● Tambua mikakati ya kutoa msaada wa kisaikolojia kwa watoto, haswa kwa wale waliowekwa karantini |

<table>
<tr><th colspan="2">Matendo ya Ulinzi wa Mtoto yanayopewa Kipaumbele</th></tr>
<tr><th>Matendo ya Utayarishaji</th><th>Matendo ya kukabiliana</th></tr>
<tr><td>● Kufanya kazi na watendaji wa afya kuunda mikakati ya kujumuisha watoto waliotengwa na wanaoishi katika mazingira ambayo si rahisi kuwafikia<br>● Kutambua hatua za kupunguza hatari kwa wahudumu wa kesi ya COVID-19 wa kesi na njia mbadala za kufatilia maendeleo ya watoto ikiwa itashindikana kuwatembelea majumbani<br>● Kuwezesha rufaa kwaajili ya huduma zingine maalumu ikiwemo huduma kwa waathirika wa Ukatili wa kijinsia.</td><td>● Kuanzisha mifumo ya kuhakikisha kuwa jamii zinazokabiliwa na vizuizi vya kutoka majumbani zinaendelea kupatikana kwa utunzaji bora wa watoto wote wanaokabiliwa na ukatili.<br>● Kutambua watoto ambao hadhi yao ya kutengwa inawapa mazingira magumu zaidi (yaani, watoto wasiotunzwa na familia; watoto ambao ni wakimbizi, wahamaji wa ndani, wahamiaji au wasio na nchi; watoto wanaoishi na / au wanaofanya kazi mitaani; watoto wenye ulemavu; nk).</td></tr>
<tr><td colspan="2">Mkakati wa Ulinzi wa Mtoto: Malezi Mbadala (Kiwango Na. 19 cha CPMS)</td></tr>
<tr><td>● Kuwatambua na kuwapa mafunzo na ushauri watendaji wa afya katika kuzuia utengano wa kifamilia na kutoa taarifa au rufaa ya watoto ambao hawana uangalizi au wametengwa.(UASC)<br>● Kuwatambua na kuwapa mafunzo wanajamii ambao wako tayari kuwatunza watoto ambao hawana uangalizi na waliotengwa katika kipindi hiki cha mlipuko wa COVID-19<br>● Kujenga uwezo wa mifumo ya idara mbalimbali kuzuia utengano na kurejesha wanafamilia waliotengwa na kuwapatia watoto wasio na uangalizi na waliotengwa uangalizi mbadala majumbani kwao.</td><td>● Kuanzisha mpangilio mbadala wa malezi, unaotegemea familia (ikiwezekana uwe baina ya watu wenye uhusiano wa damu)<br>● Kuhakikisha watoto wanaotengwa na walezi wao wanapata fursa za kuwasiliana nao kila wakati<br>● Kuepuka kusambaza habari zinazoweza kuchochea familia kupuuza au kuwatelekeza watoto wao bila kukusudia<br>● Kufanya kazi na mamlaka husika kuanzisha mfumo wa usajili kuzuia utengano wa muda mrefu na kuwawezesha kuungana na familia zao tena.</td></tr>
</table>

# 3. Marejeleo

| | |
|---|---|
| ***Marejelea juu ya eneo la uwajibikaji kuhusu ulinzi wa mtoto dhidi ya COVID-19***<br><br>*(Child Protection Area of Responsibility Child Protection Resource Menu for COVID-19)* | Makusanyo juu ya ulinzi wa mtoto kama mwitikio dhidi ya COVID-19<br><br>*(A collection of child protection resources related to a COVID-19 response)* |
| ***Jumbe na mikakati muhimu kuhusu kukabiliana na ugonjwa wa corona (COVID-19) pamoja na kuuzuia mashuleni***<br><br>*(Key messages and actions for coronavirus disease (COVID-19) prevention and control in schools)* | Mwongozo wa utendaji juu ya kuwalinda watoto na mashule dhidi ya maabukizi ya COVID-19<br><br>*(Operational guidance on protecting children and schools from COVID-19)* |
| ***Kurasa rejea ya INEE kuhusu Kirusi kipya cha Corona (COVID-19)***<br><br>*(INEE Resource Page on Novel Coronavirus (COVID-19)* | Makusanyo juu ya COVID-19 na elimu wakati wa dharura<br><br>*(A collection of COVID-19 and education in emergencies resources)* |
| ***Muhtasari rejea wa IASC MHPSS kuhusu MHPSS za COVID-19***<br><br>*(IASC MHPSS Reference Group's Briefing Note about MHPSS Aspects of COVID-19)* | Muhtasari juu ya mambo ya MHPSS ya mlipuko wa kirusi kipya cha Corona mwaka 2019<br><br>*(A briefing note about MHPSS aspects of the 2019 novel coronavirus (COVID-19) outbreak)* |